


**Muhtasari**

- Mvua Msimu zimeanza katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka na wakulima wanajishughulisha na maandalizi ya mashamba na kupanda
- Mvua zinazotarajiwa kwa kipindi cha Novemba 11-20, 2019 zitasaidia katika uotaji wa mbegu na ukuaji wa mazao
- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki
- Wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu

**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019**

**K**atika kipindi cha dikadi, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua kusogea katika eneo la kusini mwa dunia. Hata hivyo katika kipindi hiki kulitokea kuimarika kidogo kwa migandamizo mikubwa iliyopo kusini mwa dunia, na kupelekea uwepo wa vimbunga **Kyarr** na **Maha** ambavyo vilipunguza kasi ya ukanda wa mvua kuelekea kusini. Aidha hali hii ilidhoofisha pepo za kaskazi kuelekea nchini na hivo kupunguza uwepo wa mvua katika maeneo mengi. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilidhoofisha mifumo wa utengenezaji wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.



**Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Novemba 1- 10, 2019.**

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019**

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019**

**K**atika dikadi hii, vipindi vya mvua za wastani viliripotiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, kaskazini mashariki na magharibi mwa nchi na pwani ya kaskazini. Aidha mvua nyepesi iliripotiwa katika maeneo ya nyanda za juu kusini mashariki pamoja nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya kati. Maeneo mengi ya ukanda wa pwani yalipima mvua yenye kufikia mm 51 hadi 200 mm kama inavyoonekana katika ramani.

**K**atika kipindi cha dekadhi husika, wakulima katika maeneo mengi nchini waliendelea na uandaaji wa mashamba pamoja na upandaji kutokana na mvua za Vuli zinazoendelea na kuanza kwa mvua za Msimu. Hata hivyo baadhi ya maeneo ya mkoa wa Dodoma, Singida na wilaya ya Longido wakulima wanaandaa mashamba. Kwa upande wa kanda ya ziwa Viktoria hususan mkoa wa Kagera wakulima wanaendela na shughuli za palizi. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo umeimarika

katika baadhi ya maeneo yayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka kutokana na mvua za *Vuli* zinazoendelea.

**HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI  
CHA NOVEMBA 1-10, 2019**

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mtawanyiko hafifu wa mvua

**MIFUMO YA HALI YA HEWA  
INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA  
NOVEMBA 11-20, 2019**

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha kusogea kwa ukanda wa mvua katika eneo la ukanda wa kusini mwa dunia. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii itaathiri mfumo wa utengenezaji wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

**HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA  
KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019**

**M**aeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua za wastani katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro)

yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kuwa hali ya ukavu

**HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA  
KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2019**

vua zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja na miwili ya mvua zinatarajiwa kuongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa uoteshaji wa mbegu na ukuaji wa mazao. Wakulima wanashauriwa kuendelea kufatilia taarifa za siku kumi na kufata ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi stahiki ya mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo wakulima wa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka wanashauriwa kuzitumia mvua za *Msimu* zinazotarajiwa kupanda mazao pale kutakapokuwa na unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

**HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA  
KIPINDI CHA NOVEMBA 1-10, 2019**

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matumizi endelevu ya rasilimali hii.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania  
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania